BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA MBILI

Kikao cha Kumi – Tarehe 26 Septemba, 2023

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Uchumi kwa mwaka 2022/2023.

### Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Uchumi kwa mwaka 2022/2023.

### Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Uchumi Kuhusu Ripoti ya Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji juu ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Ripoti ya Kamati ya Uchumi kwa mwaka 2022/2023.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Uchumi Kuhusu Ripoti ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi juu ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Ripoti ya Kamati ya Uchumi kwa mwaka 2022/2023.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

20. MHESHIMIWA ABDALLA ABASS WADI (Jimbo la Nungwi) – Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Tunavipongeza Vikosi vyetu vya SMZ kwa juhudi kubwa ya kufungua Vituo vya Afya na Hospitali mbali mbali nchini, hali inayoonesha wazi kuwa, vikosi hivi vina mchango mkubwa kwa nchi yetu na vinatoa msaada mkubwa kwa wananchi wetu. Hata hivyo, kuna tatizo la upungufu mkubwa wa madaktari katika vituo hivyo.

(a) Je, Wizara yako inasema nini juu ya kuongeza nafasi za masomo kwa mwaka huu hasa katika fani ya udaktari, ili kuondokana na upungufu uliopo.

(b) Je, kuna mpango gani wa kuwatumia wataalamu waliostaafu, japo kwa mkataba hadi hapo madaktari waliopo masomoni watakapomaliza masomo yao.

85. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Katika kipindi cha miaka iliyopita, tulishuhudia ziara za kimafunzo ya vitendo (attachments) za Waheshimiwa Madiwani wa Zanzibar kuwatembelea Waheshimiwa Madiwani wenzao wa Tanzania bara, nao pia kuja kujifunza kwa vitendo hapa Zanzibar. Hili limefanywa kwa dhamira za kujifunza na kubadilishana uzoefu wa kazi zao za kila siku, kwa lengo la kuendeleza ujirani mwema. Hata hivyo utamaduni huo umefifia katika kipindi cha miaka ya hivi karibuni.

(a) Je, Serikali hailioni hili kuwa ni jambo lenye tija kubwa kwa mustakbali wa uendelezaji wa ujirani mwema na

uimarishaji wa utendaji wa viongozi wetu hawa.

(b) Je, ziara hizo bado zinaendelea kwa kiwango gani kwa sasa.

(c) Je, ni sababu gani zilizopelekea kusita au kufifia kwa utamaduni huo.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

115. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Je, ni kwa kiwango gani bandari zetu zinachangia kukua kwa uchumi wa Zanzibar kupitia uvuvi.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

36. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Je, ni ipi mikakati halisi ya Wizara dhamana ya kilimo ya kuhakikisha kwamba inapunguza kwa kiwango kikubwa utegemezi wa mazao ya chakula nchini kwetu.

37. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

(a) Je, kuna tathmini yoyote iliyofanywa na Wizara yako ya kuhakikisha kuwa wakulima wanaacha kutegemea mvua na kujikita katika kilimo cha umwagiliaji maji.

(b) Je, tathmini hiyo ikoje na kwa asilimia ngapi inaonesha kuwa wakulima wetu wameacha kutegemea kilimo cha kusubiria miongo ya mvua na kujikita katika kilimo cha umwagiliaji maji.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

70. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Sera ya Elimu inayosimamiwa na Wizara yako ndio inayosababisha vyeti vya kumalizia masomo ya Form II visitoke, pamoja na ukweli kuwa, wanafunzi wa kiwango hicho huyamalizia masomo yao kwa kufanya mtihani wa taifa na wanaofaulu ndio huendelea na masomo ya Form III.

(a) Je, kuna sababu zipi na tofauti ipi ya kutolewa vyeti kwa wanafunzi wanaomaliza Form II na wale wanaomaliza Form IV, wakati wote humaliza masomo yao kwa kufanya mtihani.

(b) Je, ni lini Wizara yako itairekebisha Sera yake inayohusiana na kutolewa kwa vyeti baada ya masomo ya Form II.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

54. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Utamaduni ni moyo na uhai wa taifa lolote lile duniani. Kutouthamini utamaduni wake, taifa hilo sio tu hupoteza utambulisho wake, lakini pia hukosa hadhi na thamani kutoka kwa mataifa mengine.

(a) Je, kwa kuzingatia tathmini ya maofisa utamaduni wetu, ni zipi mila za asili za Kizanzibari ambazo kwa sasa zinaelekea kupoteza uasilia wake.

(b) Je, ni ipi mikakati ya Wizara yako katika kuzihuisha tamaduni zetu ili ziweze kurejea kwenye uhalisia wake.

**<u>Wizara ya Maji, Nishati na Madini:</u>**

73. MHESHIMIWA MWANAJUMA KASSIM MAKAME (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji Nishati na Madini:

Naipongeza Serikali kwa hatua inazoendelea kuzichukuwa katika kuongeza kasi katika vyanzo vyake vya kukusanya mapato. Katika hilo, Serikali imeanzisha vituo vya ukaguzi wa maliasili zisizorejesheka katika maeneo mbali mbali nchini kwa lengo la kuzuia upotevu wa maliasili hizo. Hata hivyo, baadhi ya vituo hivyo vinakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa huduma muhimu ikiwa ni pamoja na vyoo.

(a) Je, ufahamu wa Wizara juu ya changamoto hii ukoje.

(b) Je, ni sababu zipi zilizopelekea vituo hivyo kutokuwa na vyoo vya kudumu wakati huduma hii ni muhimu kwa wafanyakazi wake.

(c) Je, ni hatua zipi za dharura Wizara itazichukuwa ili kuondosha tatizo hili.

**<u>Wizara ya Afya:</u>**

57. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Ni jambo lisilopingika kuwa, Tiba Asili zina mchango mkubwa katika kuwasaidia wananchi wetu kujikinga na kujitibu na maradhi tofauti. Hata hivyo, kwa muda mrefu tiba hizi zimekuwa zinakabiliwa na changamoto mbali mbali.

Je, kuna tafiti ngapi hadi sasa zimefanywa na Baraza la Tiba Asili ambazo kwa kiasi fulani zinaelekea kuleta mbadala wa tiba kwa baadhi ya magonjwa mbali mbali kwa jamii.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

### Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Ripoti ya Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Uchumi kwa mwaka 2022/2023.

### Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Ripoti ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Uchumi kwa mwaka 2022/2023.

**Zanzibar,**
**26 Septemba, 2023.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**